

KILOMBERO VALLEY TEAK COMPANY LIMITED
SERA YA MAZINGIRA

TOLEO LA JUNI, 2024



Utangulizi

KVTC inatambua kuwa maendeleo na shughuli zake katika bonde la Kilombero vitakuwa na athari za kimazingira katika maeneo yanayosimamiwa na kampuni. Kampuni itasimamia uendeshaji wake katika namna itakayopunguza athari mbaya. Kampuni itafuata sheria zote zilizopo. Kampuni itazingatia makubaliano husika ya kimataifa/ kikanda, mikataba na makubaliano ya kimazingira ya nchi. Kampuni itafuata Miongozo ya mfumo wa usimamizi wa mazingira (ISO14001:2015) na misingi ya kanuni za FSC inayohusiana na usimamizi wa mazingira. Kampuni itafikia lengo hili kwa kubainisha athari mbaya za kimazingira na kuanzisha programu ya kuendelea kuboresha usimamizi dhidi ya athari hizi. Ili kufikia lengo hili, kampuni itaendeshwa kulingana na misingi ifuatayo na kufuatalia utendaji wake kulingana na misingi hiyo. Shughuli za kampuni zitajumuisha kiwanda cha kuchakata mbao, utunzaji mashamba ya miti, bustani ya miti, uvunaji wa miti na usafirishaji.

Sera

KVTC itaongeza uhifadhi wa viumbe anuwai katika ardhi wanayoitumia. Eneo muhimu la ardhi litasimamiwa kwa lengo la msingi la kuendeleza eneo la Miombo linalohusiana na viumbe anuwai. Viumbe adimu, walio hatarini, wanaolindwa na maeneo yenye viumbe anuwai wengi yatabainishwa na kulindwa dhidi ya uharibifu. Mtandao wa uwakilishi wa aina za makazi utatunzwa. Vikwazo dhidi ya utembeaji huru wa wanyama na mimea vitapunguzwa.

Kutakuwa na mchakato wa kubainisha maarifa mapya kuhusiana na nyanja za mazingira ya misitu endelevu katika savana ya tropiki.

Miti ya Kigeni kwenye uoto wa asili itazuiwa isienee kukinga uonekanaji vizuri wa uoto wa asili.

Matumizi ya moto ya kampuni yatarekebishwa kwa karibu kadri iwezekanavyo kwa kufuata mifumo ya asili ya uoto.

Kampuni itapunguza athari zake kwenye kiasi na ubora wa vyanzo vya maji. Hatua zitachukuliwa kuzuia uchafuzi wa vyanzo vya maji kwa vifaa vinavyotumiwa kwenye shughuli za misituni. Upotevu wa ubora wa maji kutokana na uzibaji maji kwa tope usio wa asili kutoka kwenye barabara za kampuni, chemba za uoto na maeneo mengine ya kampuni utapunguzwa. Athari kwenye kiasi cha maji zitabainishwa na inapobidi hatua za usimamizi zitabadilishwa ili kuendelea kuwa mtiririko wa vijito.

Kampuni itaendeleza uzalishaji wa msingi wa rasilimali yake. Mmomonyoko wa udongo unaosababishwa na shughuli za misituni utapunguzwa. Hadhi ya virutubishi vya udongo wa misitu itaendelezwu kwa mzunguko wa kufuatana.

Kampuni itapunguza matumizi yake ya kemikali na mafuta, kuyatumia kwa namna inayofaa na kuzuia utapakaaji wake kwenye maeneo yanayozunguka. Vitu vichafu vitashughulikiwa kwa namna inayofaa. Kemikali zitatumika tu kama sehemu ya namna jumuishi ya utatuzi wa tatizo. Kemikali zitahifadhiwa, kusafirishwa na kutumiwa katika namna itakayopunguza hatari ya uchafuzi. Kemikali chafu, mafuta na oili zitarejelezwa au kutupwa kwenye eneo lilitengwa kwa ajili hiyo. Uchafu utaondolewa kwenye mfumo wa uoto na kutupwa sehemu inayostahili.

Shughuli za uvunaji na usafirishaji vitapangwa na kutekelezwa kulingana na viwango bora vya uendeshaji vya kiwanda ili kuhakikisha athari ndogo kwenye mazingira.

Kiwanda cha uchakataji na miundombinu inayohusiana vitasimamiwa kulingana na kanuni kama zilivyowekwa kwenye nyaraka za miongozo na Tathmini ya Athari ya Mazingira.

Kampuni itasimamia maendeleo ya nyanja za kimazingira za uendeshaji wake na ikibidi kuvijumuisha hivi kwenye programu zake za usimamizi wa mazingira.

Kampuni itaainisha mahitaji ya wadau husika na changamoto za ndani na nje ya Kampuni zinazoathiri ufanisi wa mfumo wa usimamizi wa mazingira na kuzishughulikia kulingana na taratibu za Kampuni.

Kutakuwa na mchakato wa kuanda matokeo ya ufuutilaji unaoongozwa na kampuni kwa ajili ya uhakiki wa usimamizi. Uhakiki wa mara kwa mara wa usimamizi utahakikisha kuwa maarifa mapya yanajumuishwa katika shughuli za usimamizi wa misitu.


Irvine Kanyemba - Mkurugenzi Mtendaji